Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MTIHANI WA UTAMILIFU SHULE ZA SEKONDARI WILAYA YA MWANGA (MWASSES)
KIDATO CHA NNE 2020

MSIMBO: 021 **KISWAHILI**
MUDA: SAA 3:00 **Jumanne 29, Septemba 2020 Mchana**

MAELEKEZO

1) Karatasi hii ina sehemu A, B and C zenye jumla ya maswali kumi na mbili (12)
2) Jibu maswali yote katika sehmu A na B na maswali matatu (03) kutoka sehemu C
3) Zingatia maagizo ya kila sehemu na kila swali
4) Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa karatasi

SEHEMU A {Alama 15 }

Jibu maswali yote

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi yako ya kujibia.

i. Tuimbe sote ni
   a) Wingi nafsi ya kwanza
   b) Wingi nafsi ya pili
   c) Umoja nafsi ya kwanza
   d) Umoja nafsi ya pili
   e) Wing nafsi ya tatu

ii. Kusoma kwake kwa bidii kumempatia mafanikio, Neno lililopigiwa mstari ni:
   a) Kitenzi
   b) Kitenzzi kisaidizi
   c) Kitenzi jina
   d) Kitenzi kikurupushi
   e) Nomino

iii. Jozi ipi ina vipengele sahihi vinavyounda umbo la ndani la kazi ya fasihi simulizi
   a) Falsafa, muundo, ujumbe, wahusika
   b) Mandhari, msimamo, ujumbe, dhamira
   c) Ujumbe, mtizamo, migogoro, dhamira
   d) Ujumbe, msimamo, dhamira, wahusika
   e) Lugha, migogoro, falsafa, mtindo

iv. Mpangilio sahihi wa vipashio vinavyounda lugha ya kiswahili ni upi
   a) Mofimu, kishazi, kirai, neno na sentensi
   b) Mofimu, neno, kirai, sentensi na kishazi
   c) Neno, kirai, kishazi, sentensi na mofimu
   d) Neno, mofimu, kirai, kishazi na sentensi
   e) Mofimu, neno, kirai, kishazi na sentensi

v. Ni jambo gani linalodhihirisha upekee wa kazi Fulani ya kifasihi
   a) Muundo wa kazi husika
   b) Wahusika wa kazi husika
   c) Jina la kazi husika
   d) Jina la mtunzi husika
   e) Mtindo wa kazi husika

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

vi. Ipi ni sehemu Ndogo sana ya lugha?
   a) Mofimu
   b) Neno
   c) Herufi
   d) Silabi
   e) Mofoloji

vii. Ni taratibu zipi zinazofuatwa na lugha fasaha:
   a) Kimaana, kimatamshi, kilafudhi, kimuundo
   b) Kimatamshi, kimofolojia, kiufundi, kimaana
   c) Kimatamshi, kimaana, kimuundo, kimantiki
   d) Kimantiki, kifonolojia, kimaana, kilafudhi
   e) Kilafudhi, kimuundo, kiufundi, kimaana

viii. Kwa nini lugha ni sauti za nasibu_____
   a) Kwa sababu inatumia ishara
   b) Kwa sababu intumia sauti
   c) Kwa sababu inabeba maana
   d) Kwa sababu inatumiwa na wanyama
   e) Kwa sababu inatumiwa na binadamu

ix. Ni sifa ipi hutofautisha fasihi simulizi na fasihi andishi?
   a) Ukubwa
   b) Ueneaji
   c) Uwasilishaji
   d) Uhifadhi
   e) Utamkaji

x. Mhakiki wa kwanza katika kazi ya fasihi simulizi mfano wa igizo ni:
   a) Mtunzi
   b) Mtazamaji
   c) Msomaji
   d) Mwigizaji
   e) Mfasili

2. Oanisha maana za dhana za uandishi zilizo katika orodha A kwa kuchagua herufi ya dhana husika katika Orodha B, Kisha andika herufi husika katika karatasi yako ya kujibia:

ORODHA A	**ORODHA B**
i. Irabu ii. Sarufi iii. Sentensi sahili iv. Kidahizo v. Chagizo	A. Kiwakilishi cha a – unganifu B. Tanzu ya lugha C. Maana ya msingi D. Inaotamkwa huwa hakuna kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa E. Ina hadhi ya kishazi huru F. Kitomeo na taarifa zake G. Ni maneno yanayotokea baada ya kitenzi na kufanya kazi kama kielezi.

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

SEHEMU B (Alama 40)

3. Kwa kutumia mifano dhabiti fafanua dhana zifuatazo
    a) Urudufishaji
    b) Uambishaji
    c) Kutohoa maneno
    d) Ngeli

4. Maneno huweza kubadilika kutoka aina moja na kuwa aina nyingine “Dhihirisha kaulli hii kwa kubadili maneno yafuatayo kwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika mabano
    a) Kwenda (Badili kuwa nomino)
    b) Ogopa (Badili kuwa kivumishi)
    c) Mzazi (Badili kuwa kitenzi)
    d) Linda (Badili kuwa nomino)
    e) Bisha (Badili kuwa kivumishi)
    f) Bora (Badili kuwa kitenzi)
    g) Refu (Badili kuwa kitenzi
    h) Kabati (Badili kuwa kielezi)

5. Kwa kutumia mifano kuntu fafanua tabia zisizopungau nne (4) za vitenzi vya kiswahili

6. Wewe na msaidizi wako mmehudhruria kikao cha kupanga mahafali ya kidato cha nne. Andika kumbukumbu ya kikao kilichofanyika katika shule yenu.

7. Baada ya kiswahili kuteuliwa kuwa lugha ya Taifa vyombo mbalimbali viliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza kiswahili dhibitisha dai hilo kwa kutumia asasi tatu (03)

8. **Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata**

    1) Korona ugonjwa gani umezua taharuki;
    Chanjo haipatikani Ulaya hakukaliki,
    Tiba haijulikani, Dunia haifurukutu,
    Korona ni maafa kujikinga lazima,

    2) Hofu kubwa imetanda, wakubwa kwa wadogo;
    Mafua, homa kupanda utaona uki”gugo”,
    China mpaka mpanda, korona haina vigo,
    Korona ina maafa kujikinga lazima

    3) Walakini juu ya yote, mapenzi yameoteshwa,
    Karantini kwa wotee, makapera wameoa,
    Mabinti wasiopenzini, huu msimu wa ndoa
    Korona ina maafa kujinginga lazima

Search ⇢ www.africona.net

Visit: www.africona.net/Teacher pizo for Free Past Papers and Notes.

4) Hakika baniani mbaya Kiatu chake dawa,
Wanandoa walishane penzi bila taabu,
Nao wapenzi wachanga, wasubiri janga lipite
Korona ina maafa kujikinga lazima

5) Mungu atasaidia Korona itaisha,
Elimu tazingatia Wizara wanakumbushia,
Tunawe yetu mikono, epuka msongamano
Koroana ina maafa kujikinga lazima

MASWALI

a) Pendekeza kichwa cha habari kisichozidi maneno matatu
b) Unafikiri kwa nini mshairi anatuasa kuwa Korona ina maafa kujikinga lazima?
c) Mashairi wa shairi hili anawashauri nini wanafunzi kuhusiana na suala la mapenzi?
d) Kutokana na shairi ulilosoma eleza njia tano unazozijua utakazotumia kuepukana na ugonjwa wa Korona

SEHEMU C (Alama 45)

Jibu maswali matatu (3) kutoka katika sehemu hii

9. Fasihi simulizi ndio fashihi ya awali iliyoanza wakati binadamu alipoanza kutumia lugha mara kwa mara inapowasilishwa kwa hadhira huchukua sifa muhimu ambazo sirahisi kuziona katika fasihi Andishi. Dhibitisha ukweli huu kwa kutumia hoja tano.

10. Nyimbo ni mbinu ya kifasihi ambayo wasanii wengi hutumia ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Dhibitisha usemi huu kwa kutumia waandishi wawili wa riwaya ulizosoma.

11. Taswira ni kibebeo cha ujumbe wa mwandishi katika jamii. Jadili kauli hii kwa kutumia thamthiliya mbili ulizosoma.

12. "Mshairi siku zote hukemea uonevu katika jamii "dhibitisha kauli hii wa kutoa hoja tatu kutoka katika kila diwani kati ya Diwani mbili (2) ulizosoma.

ORODHA YA VITABU

USHAURI

Wasakatonge	-	M.s Khatibu (DUP)
Malenga wapya	-	Takiluki (DUP)
Mashairi ya chekacheka	-	T. A Mvungi (EP & D. LTD)

RIWAYA

Takadini	-	Benj. Hanson (MBS)
Watoto wa mama ntiliye	-	E. Mbogo (H.P)
Joka la mdimu	-	A.J Safari (H.P)

TAMTHILIYA

Orodha	Steven Reynolds (MA)
Ngoswe penzi kitovu cha uzembe	-E. semzaba
Kilio chetu	-Medical Aid foundation

Search ⇢ www.africona.net